

# Haki za mtoto

Kila mtoto ni sawa na ana haki sawa." Haki" ni vipengee ambavyo kila mtoto anastahili kuwa navyo ama kuvifanya. Haki hutoa mwelekeo kuhusu yale yaliyo mazuri kwa watoto katika hali tofauti tofauti na kutufahamisha yale yaliyo ya muhimu ili kujinasua kutoka kwa madhara. Karibu kila taifa duniani limekubaliana na haki zilizo nukuliwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa (United Nations Covention), kuhusu haki za mtoto. unapokua, utaweza kufanya maamuzi yako kibinafsi, na pia kuwakilisha haki zako.

1

Kila mtu chini ya umri wa miaka 18 anastahiki haki zote katika mkataba kuhusu haki za mtoto. Kuanzia sasa tutairejelea kama CRC.

2

Haki hizi zinafaa kutumika kwa kila mtu na hakuna mtoto ambaye atahudumiwa visivyo kwa msingi wowote. Haijalishi taifa, dini, uwezo, jinsia au hata familia uliyotoka.

3

Watu wote wazima ni sharti wafanye yale yote yaliyo bora kwako, na pia wafikirie jinsi uamuzi wao unavyo kuadhiri.

4

Serikali ina jukumu la kuhakikisha kwamba haki zako zinalindwa. Ni sharti wasaidie jamii yako kulinda haki zako.

5

Familia yako inajukumu ya kukusaidia wewe kujifunza na kutumia haki zako na kuhakikisha kwamba zinalindwa.

6

Una haki ya uhai. Serikali ni lazima ihakikishe kua watoto wanaishi na kua kiafya.

7

Una haki ya jina, na jina lako sharti lijulikane rasmi na serikali. Lazima pia uwe na haki ya utaifa.

8

Una haki rasmi ya rekodi inayokutambulisha-utambulisho. Hamna anayeweza kupokonya utambulisho wako.

9

Una haki ya kuishi na mzazi au wazazi wako, mradhi isiwe mbaya kwako. Uko na haki ya kuishi na jamii inayo kutunza..

10

Iwapo unaishi taifa tofauti na la wazazi wako, una haki ya kuruhusiwa kutembelewa na wazazi wako, kua katika mawasiliano na pia kukutana pamoja kama familia.

11

Una haki ya kulindwa kutokana na utekaji nyara.

12

Uko na haki ya kupata maelezo na kushiriki maoni yako na wengine. Unaeza fanya hivyo kwa kuchora, kuandika ama kuingea, mradi yasiwe yenye kuumiza mtu yeyote.

13

Una haki ya kueleza maoni yako watu wazima wanapofanya maamuzi yanayokuhusu wewe. Watu wazima ni sharti wayasikize na kuyazingatia maoni yako.

14

Una haki ya kuwaza na kuamini unachotaka na kuiga dini utakayo. Ni jukumu la wazazi wako kusaidia kuamua kati ya sawa na mbaya na gani bora zaidi kwako.

15

Una haki ya kuchagua rafiki na kujiunga ama kuunda vikundi au vilabu, bora visiwe vya kudhuru wengine.

16

Una haki ya usiri.

17

Una haki ya kupata maelezo yaliyo muhimu kwa ustawi wako. Maelezo yanaeza kuwa kwenye redio, gazeti, vitabu, tarakilishi na vyanzo vingine. Watu wazima ni sharti kuakikisha maelezo hayana madhara kwako. Ni muhimu pia kwao kusadia wewe kuelewa maelezo unayohitaji.

18

Una haki ya kukuzwa na kulindwa na mzazi mmoja au wote ikiwezekana. Ni muhimu kwa wazazi wako kuzingatia kilicho bora kwako.

**19** Una haki ya utunzaji maalum na usaidizi iwapo wazazi wako hawawezi kutunza.

**20** Una haki ya kulindwa na kusaidiwa iwapo wewe ni mtoto mkimbizi na hauna chaguo ila kutoka nyumbani kwenu hadi taifa lingine. Watoto wakimbizi wana haki zingine zote katika CRC.

**21** Ni lazima upokee utunzaji maalum na usaidizi, kama vile elimu maalum, iwapo una ulemavu ndiposa uishi maisha kamili na bila kutegemea.

**22** Una haki ya kupata huduma ya afya bora, maji safi, chakula chenye madini bora na mazingira safi ndipo uishi kiafya. Mataifa tajiri ni sharti wasaidie mataifa maskini ili kufikia haya matarajio.

**23** Iwapo unalindwa na serikali ya majimbo, badala ya wazazi, una haki ya hali yako kuchunguzwa mara kwa mara.

**24** Una haki ya kiwango cha kuishi ambacho ni bora kwa kutimiza mahitaji yako. Inajumuisha; haki ya chakula, mavazi na mahali salama pa kuishi.

**25** Una haki ya kuhudumiwa vizuri na kulindwa kutokana na kuumizwa ama kutendewa mabaya.

**26** Iwapo unahudumiwa na wazazi wa kambo una haki ya kutunzwa na kulindwa.

**27** Una haki ya usaidizi kutoka kwa serikali iwapo wewe ni fukara.

**28** Una haki ya elimu ya kiwango cha hali ya juu. wahitaji kutiwa moyo ili kuhitimu kiwango cha juu cha elimu kulingana na uwezo wako.

**29** Elimu ni sharti ikusaidie kuendeleza utu, vipaji na uwezo. Ni lazima pia ikuhimiza kuheshimu wazazi wako, wewe binafsi na watu wengine.

**30** Una haki ya kujifunza na kutumia lugha yako, mila na dini, hata kama haishiriki na wengi wa watu katika taifa unaloishi.

**31** Una haki ya kupumzika na kucheza.

**32** Una haki ya kulindwa kutokana na kazi zenye madhara kwako na zinazo kudhuru kiafya na kielimu. Iwapo utafanya kazi, una haki ya kulipwa vizuri na kuwa salama.

**33** Una haki ya kulindwa kutokana na madawa ya kulevywa na biashara za madawa ya kulevywa.

**34** Una haki ya kuwa huru kutokana na unyanyasaji wa kijinsia.

**35** Hakuna yeyote anayekubaliwa kukuteka nyara ama kukuuzwa.

**36** Una haki ya kulindwa kutokana na unyanyasaji wa namna yeyote.

**37** Hakuna anayeruhusiwa kukuadhibu kikatili ama kwa njia inayokudhuru kwa nama yoyote ile.


**38** Una haki ya kulindwa na kua huru kutokana na vita. Watoto chini ya umri wa miaka 15 hawawezi jiunga na jeshi au kushiriki vita.

**39** Una haki ya kusaidiwa iwapo umeumizwa, kupuuzwa ama kutunzwa vibaya.

**40** Una haki ya kupewa usaidizi wa kisheria na kutunzwa vyema katika mfumo wa sheria.

**41** Iwapo sheria za taifa unaloishi ni bora kuliko makala yaliyopo katika CRC, basi hizo sheria zitatumika.

**42** Una haki ya kujua haki zako na watu wazima ni sharti wakusaidie kuzifahamu.

 Nakala 43 hadi 54 inaelezea vile serikali na mashirika ya kitaifa yatahakikisha kwamba watoto wanalindwa kando na haki zao.